# LONDA

## MALAWI HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE






## RIPOTI YA 2020

www.paradigmhq.org

PARADIGM INITIATIVE

@ParadigmHQ

# LONDA

**MALAWI HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI**

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

**Imechapishwa na Paradigm Initiative**
374 Borno Way, Yaba, Lagos, Nigeria
Email: media@paradigmhq.org
www.paradigmhq.org

Iliyochapishwa mnamo Aprili 2021

Ripoti iliyotolewa na Donald Flywell Malanga
Timu ya Uhariri: 'Gbenga Sesan, Kathleen Ndongmo, Koliwe Majama, Margaret Nyambura Ndung'u, Mawaki Chango, Nnenna Paul-Ugochukwu and Thobekile Matimbe.
Ubunifu na Luce Concepts

This publication may be reproduced for non-commercial use in any form provided due credit is given to the publishers, and the work is presented without any distortion.

Copyright © 2021 Paradigm Initiative

Creative Commons Attribution 4.0 International (CC BY 4.0)



# LONDA

**MALAWI HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI**

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

Asasi za kiraia zinaendelea kufanya kazi ili kuendeleza haki za dijitali na ujumuishi barani Afrika, kuhakikisha njia bora zinapitishwa katika sera na sheria. Ripoti hii inachambua hali ya haki za dijitali na ujumuishi nchini Malawi, ikichunguza ukiukaji na mapungufu, ikiangazia utumiaji na utekelezwaji wa sera na sheria, ikiangazia hatua muhimu na kutoa mapendekezo kwa mandhari ya dijitali nchini Malawi. Pamoja na ripoti kutoka nchi 20, toleo hili linaangazia kati ya maswala mengine, pengo la kidijitali lililozidishwa na janga la COVID-19 na kufichua ukiukaji kwenye nyanja tofauti kama vile faragha, ufikiaji wa habari, na uhuru wa kujieleza na msingi wa sheria na sera ulioelezewa vizuri .

PARADIGM INITIATIVE

@ParadigmHQ

## YALIYOMO


UTANGULIZI 1

MAZINGIRA YA KISIASA NA HAKI ZA KIDIJITALI 2

MTANDAO NA UFIKIAJI TEHAMA 2

UHURU WA KUJIELEZA NA UFUATILIAJI MTANDAONI 3

FARAGHA YA DATA, ULINDAJI, NA UTAMBULISHO WA KIDIJITALI 4

ATHARI YA KANUNI ZA COVID -19 KWA HAKI ZA KIDIJITALI 5

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 6



Malawi ni taifa lililozungukwa na nchi kavu linalopakana na Tanzania, Zambia, na Msumbiji. Nchi hii ina idadi ya watu inayokadiriwa kuwa watu million 17.7, 85% yao wakisemekana kuishi maeneo ya vijijini.[1] Pato linalozalishwa ndani ya nchi na raia waliomo ndani ya nchi husika (GDP) kwa kila raia linakadiriwa kuwa dola za Marekani $516.80.[2]

UTANGULIZI

# HAKI ZA DIJITALI NA UJUMUISHAI YA NCHI YA DEMOKRASIA YA MALAWI

Wanawake wengi wako kwenye sekta ya kilimo ambacho ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Malawi. Kati ya wale walio kwenye ajira isiyo na kilimo, 21% ni wanawake na 79% ni wanaume na idadi imesalia kuwa ileile kwa miaka sasa. Licha ya mageuzi anuwai ya kimuundo katika miaka ya hivi karibuni, Malawi inaendelea kuorodheshwa kama mojawapo wa nchi zenye maendeleo duni ulimwenguni, inayoathiriwa kila mara na viwango vya juu vya umaskini na udhaifu wa mabadiliko ya hali ya tabianchi kama vile mafuriko na mvua ya masika.

Ujio wa mtandao na ukuaji kwa kasi ufikiaji wake na Teknolojia za Habari na Mawasiliano (TEHAMA),[3] kumefanya haki za kidijitali kuwa za lazima kufuatia jinsi watu duniani kote wanavyotumia na kufurahia haki za kimsingi za binadamu.[4] Malawi, kama nchi zinginezo barani Afrika, imetunga sheria kadha zilizopo na vifungu kuhusu haki za kidijitali.[5] Vifungu hivi vinatambua kuwa zile haki walizonazo watu nje ya mtandao, kama vile uhuru wa kujieleza, ufikiaji habari, na haki ya faragha, lazima zilindwe kwenye nyuga za mtandaoni.

**Ufikiaji habari**

1. World Bank. (2020). World Bank Indicators. http://data.worldbank.org/indicator/SP.POP.TOTL
2. World Bank. (2019). World Bank Indicators. http://data.worldbank.org/indicator/SP.POP.TOTL
3. https://www.gp-digital.org/wp-content/uploads/pubs/african-declaration-a-positive-agenda-for-rights-online.pdf
4. https://cipesa.org/?wpfb_dl=287
5. https://africadigitalrightshub.org/wp-content/uploads/2020/03/Data-Protection-Code-of-PracticeEnglish-Soft-Copy.pdf

Utafiti huu unatumia mapitio ya maandishi na mahojiano kutoa uelewa kuhusu midahalo ya hivi sasa na maswala yanayohusiana na hali ya haki za kidijitali nchini Malawi. Makala yanachambua mwelekeo wa sera kwa haki za kidijitali haswa zile zinazotawala sekta ya mawasiliano, vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, faragha na usalama na utekelezaji sheria. Makala haya yanajadili mada teule zinazohusiana na ufikiaji mtandao na miundombinu; athari ya kanuni za covid-19 kwa haki za kidijitali; na faragha, vitambulisho vya kidijitali na ufuatiliaji.

## MAZINGIRA YA KISIASA NA HAKI ZA KIDIJITALI

Malawi ni nchi ya vyama vingi na imekuwa yenye amani. Mnamo Mei 2020, nchi hiyo iliweka historia pale uchaguzi wa urais uliporudiwa tena baada ya matokeo ya awali ya Mei 2019 kufutiliwa mbali na Makakama ya Kikatiba. Mgombea wa upinzani, Dk. Lazarus Chakwera, chini ya muungano wa kisiasa "Muungano wa Tonse", alishinda uchaguzi wa urais kwa asilimia 58.9%. Ubatilishaji huo ulikuja baada ya miezi kadhaa ya maandamano endelevu ya raia dhidi ya udanganyifu wa uchaguzi uliogubikwa na kasoro tele.

Maandamano mengi yaliongozwa na Muungano wa Watetezi wa Haki za Binadamu (HRDC).[6] Walipanga na kueneza ujumbe wao kwa kutumia mitandao ya kijamii kama vile WhatsApp, Facebook, na Twitter. Kufuatia hilo, Malawi ilijizolea sifa kimataifa kama kinara wa demokrasia kwa kuwa wa pili barani Afrika kurudia uchaguzi wake wa urais baada ya kufutiliwa mbali kwa matokeo ya awali na mahakama kuu, na kwa mara ya kwanza kabisa katika historia kwa mgombea urais wa upinzani kushinda uchaguzi.



## MTANDAO NA UFIKIAJI TEHAMA

Licha ya ushindi mkubwa wa demokrasia nchini mnamo 2020, Wamalawi bado wanakabiliwa na changamoto za vitisho kwa haki za binadamu katika nyanja za kidijitali. Takwimu za Muungano wa Kimataifa wa Teknolojia ya Mawasiliano (ITU) zinaonyesha kuwa 14% ya idadi ya watu hutumia mtandao nchini Malawi wakati 52% wana simu za rununu. Ufikiaji wa huduma ya mtandao (broadband) ya rununu inakadiriwa kuwa 25.5% na huduma ya kudumu ya mtandao ni 0.06%.[7] Pia kuna utofauti mkubwa wa usawa wa kijinsia linapokuja kwenye suala la umiliki wa TEHAMA nchini. Karibia wanawake 34.2% wanamiliki simu ya rununu, 3.9% wanamiliki kompyuta ya mezani, wakati 5.2% tu yao wana ufikiaji wa mtandao ikilinganishwa na wenzao wa kiume.[8]

Vivyo hivyo, 3.0% ya idadi ya watu ina ufikiaji mtandao kwenye maeneo ya vijijini ikilinganishwa na 24.3% ya idadi ya mjini. Ufikiaji Kompyuta kwenye maeneo ya vijijini inasalia kuwa 2.1% ikilinganishwa na 19.2% maeneo ya mjini. Nchini Malawi, Airtel (Mw) na Telecom Networks Malawi wanasalia kuwa watoa huduma wakuu wa

6. https://afrobarometer.org/publications/ad354-malawians-support-2019-post-election-demonstrations-split-government-power-limit
7. https://www.itu.int/net4/ITU-D/idi/2017/
8. https://giswatch.org/sites/default/files/gisw2019_web_malawi.pdf

kipekee wa huduma ya mtandao wa kudumu. Mamlaka ya Mawasiliano ya Malawi (MACRA) inadhibiti sekta ya mawasiliano nchini.

Ufikiaji duni wa huduma za TEHAMA kama vile mtandao kwa kiasi kikubwa unachangiwa na miundombinu duni ya TEHAMA na ada kubwa ya kodi iliyowekewa huduma za TEHAMA. Hizi ni pamoja na kodi ya ongezeko la thamani la 16.5% (VAT) kwenye huduma za mtandao, VAT 17.5% kwenye simu na huduma, na 10% kwa ushuru wa bidhaa kwenye ujumbe wa maandishi ya simu na uhamishaji wa data ya rununu.[9] Gharama inaathiri ufikiaji mtandao kwa Wamalawi wengi. Kwa mfano, kifurushi cha data cha kila mwezi cha Gigabaiti 10 (GB) hugharimu $ 21 na Airtel na Telecom Networks Malawi (TNM). Gharama hii ni sawa na nusu ya kiwango cha chini cha mshahara wa kila mwezi wa Wamalawi wengi. Kwa kuongezea, Kielelezo Jumuishi cha Mtandao 2020, ambacho kinapima unafuu wa mtandao, upatikanaji, umuhimu wa maudhui na utayari, kinaiorodhesha Malawi katika nafasi ya 97 kati ya nchi 100.

## UHURU WA KUJIELEZA NA UFUATILIAJI MTANDAONI

Sheria ya Miamala ya Kielektroniki na Usalama wa Mtandaoni ya 2016 inazuia ushiriki wa raia kwenye nyuga za kidijitali.[10] Ibara ya 24 (2) (e) ya Sheria inasema kuwa mawasiliano kwenye mtandao yanaweza kuzuiliwa ili "kulinda utulivu na usalama wa kitaifa,"[11] wakati Ibara ya 24 (2) (f) inasema kuwa mawasiliano mtandaoni yanaweza kuzuiliwa ili "kuwezesha kizuizi cha kiufundi kwa ufikiaji wa wa mawasiliano mtandaoni". Vile vile, Ibara ya 31 (1) ya Sheria inahitaji "watoaji wa maudhui mtandaoni kuonyesha wazi kwenye ukurasa wao wa wavuti jina kamili, makazi, nambari ya simu, anwani ya barua pepe ya mhariri ikiwa ni mtu wa asili; na kwa upande wa taasisi halali jina la shirika, anwani ya posta na ya ofisi iliyosajiliwa, nambari ya simu na anwani ya barua pepe na nambari ya usajili ya mhariri".[12]

Kifungu hiki kinatoa adhabu ya faini au kifungo cha juu cha miezi 12 gerezani, na kinaweka vizuizi kwa usimbuaji fiche (encryption). Kifungu hiki pia ni sawa na cha Ibara ya 3 ya Sheria ya Uchapishaji na Utangazaji, 1947. Ingawa, hakuna mtu yeyote aliyewahi kushtakiwa kwa kifungu hiki, uwepo wake unazuia haki za raia kutokujulikana, pia kifungu hichi kina adhabu kali ya kifungo cha miezi 12 na faini nzito ya MWK 5000,0000 ($ 6,600).

Mbali na sheria hizi, pia kuna sheria zingine kandamizi ambazo zilirithiwa kutoka kwa utawala wa kikoloni wa Uingereza (1891-1964), na kipindi cha enzi ya mfumo wa chama kimoja (1964-1994), ambazo zinatishia kukandamiza ushiriki wa raia wote wa Malawi nje na ndani ya mtandao. Kwa mfano, Ibara za 50 na 51 za Kanuni ya Adhabu, ambazo zinaelezea kuhusu makosa ya uhalifu wa uchochezi, huku Ibara ya 4 ya Sheria inayolinda, Bendera na Nembo, Majina, inaelezea kuwa kosa "kufanya kitendo au kutamka maneno yoyote au kuchapisha maandishi au usemi wowote wenye lengo la kutukana, kubeza au kuonyesha kutokuheshimu "kwa" rais, bendera ya taifa, alama za silaha, muhuri wa umma au nembo yoyote iliyolindwa au chochote kile chenye mfano wake"[13] Sheria hizi kwa njia moja au nyingine zimeendeleza ukiukwaji wa haki za kidijitali nchini Malawi. Ukiukwaji wa haki za kidijitali umekua wa aina nyingi ikiwemo pamoja na kuzuia ufikiaji mtandao, uhalifishaji wa aina zingine za mawasiliano

9. Kaiyatsa.M.(2020, August). Digital rights remain under threat in Malawi despite historic win for democracy. https://advox.globalvoices.org/2020/08/05/digital-rights-remain-under-threat-in-malawi-despite-historic-win-for-democracy/
10. https://crm.misa.org/upload/web/e-transactions-act-2016.pdf
11. https://crm.misa.org/upload/web/e-transactions-act-2016.pdf
12. https://crm.misa.org/upload/web/e-transactions-act-2016.pdf
13. https://crm.misa.org/upload/web/17-laws-of-malawi-protected-flag-emblems-and-names.pdf

mtandaoni, na ufuatiliaji mtandaoni na vyombo vya dola.[14]



> ***Ukiukwaji wa haki za kidijitali umekua wa aina nyingi ikiwemo pamoja na kuzuia ufikiaji mtandao, uhalifishaji wa aina zingine za mawasiliano mtandaoni, na ufuatiliaji mtandaoni na vyombo vya dola.***

## FARAGHA YA DATA, ULINDAJI, NA UTAMBULISHO WA KIDIJITALI

Faragha ya Data na ulindaji wake unasalia kuwa swala kizushi nchini. Idara za serikali kama vile Uhamiaji, Kitengo cha Trafiki, Idara ya Taifa ya Usajili (NRB), Tume ya Uchaguzi ya Malawi (MEC), Shirika la Takwimu la Taifa (NSO), na taasisi zinazotoa huduma kama vile hospitali na taasisi za elimu, na pia benki zinapoendelea kukusanya data chungu nzima za umma.[15] Hivi karibuni, makampuni ya simu nchini yamekuwa yakikusanya data tele, haswa kufuatia kuanzishwa kwa usajili wa lazima wa kadi za simu kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Mawasiliano ya Malawi ya 2016. Walakini, hakuna twakwimu zilizopo kuhusu kiasi cha taarifa ambacho kila mojawapo wa vyombo hivi vinakusanya au ni kwa jinsi ipi vinaendeleza ukusanyaji huu kwa mujibu wa sheria zilizopo kama vile Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, 2016 na Sheria ya Upatikanaji wa Habari, 2016. Kwa kuongezea, Wamalawi wengi wa kawaida hawana ufahamu wa athari ya ukusanyaji wa vitambulisho vya kidijitali kwa faragha yao.

Kwa kuongezea, Malawi haina sheria ya faragha na ulindaji data.[16] Kwa hivyo, faragha ya data na ulindaji wa data za umma unaendelea kuwa katika hali ya hatari, hali ambayo inakiuka haki za kidijitali. Vile vile, ukosefu wa sheria halisi za ulindaji data nchini pia unamaanisha kuwa hakuna hata chombo kimoja chenye majukumu ya kudhibiti ukusanyaji wa data za kibinafsi nchini.

14. https://www.state.gov/reports/2019-country-reports-on-human-rights-practices/malawi/
15. https://www.researchgate.net/publication/341151585_State_of_Internet_Freedom_in_Malawi_2019_Mapping_Trends_in_Government_Internet_Controls_1999-2019
16. https://www.researchgate.net/publication/335136113_State_of_Internet_Freedom_in_Malawi_Privacy_and_Personal_Data_Challenges_and_Trends_in_Malawi?_sg=eL8QxUyOjJcWRRsr_lcfz8IwzG9-NEJiXsxeSvke9x4uoR3VNhfC_YojYHfad9B07TtbQivjH2nyA3spuZJo-11Q_Qvpe4PaaOWnzCOX.gJBACMVxEB4mFX1tfP8Q6QlLTfBHKf1s-Q9CVzPz1Tm--E6eu1CY7lkvXhSsJo80gQErUf9g4UJwzetsAWYqX

## ATHARI YA KANUNI ZA COVID – 19 KWA HAKI ZA KIDIJITALI

Kama nchi zingine ulimwenguni, Malawi haikusazwa na janga la COVID-19. Simu za rununu, mtandao, mitandao ya kijamii, na majukwaa mengine ya kidijitali ambayo yalitakiwa kuwezesha uwezeshwaji wa wanawake na wasichana, badala yake yakawa silaha dhidi yao. Kufuatia kufungia watu kusafiri ikiwemo na hatua zinginezo zilizowekwa na serikali, wanawake na wasichana wengi walihangaishwa mtandaoni kwa mbinu kama vile unyatiaji, unyanyasaji, kukashifiwa na uonevu wa kimtandao miongoni mwa mbinu nyinginezo.[17] Swala hili limepewa umakini mdogo licha ya kuwa linazidi kukithiri kwa kiwango ambacho hakijawahi kushuhudiwa nchini.[18]

Ingawa ukiukwaji wa haki za kidijitali unaendelea kuangaziwa katika ajenda ya kitaifa na ya ulimwengu, mnamo 2020, tumeshuhudia serikali ya Malawi ikitoa ahadi kadha za kuendeleza haki za binadamu katika nyuga za kidijitali kwenye suala hili. Mara tu baada ya Rais Chakwera kuapishwa kama Rais wa 6 wa Jamhuri ya Malawi, aliahidi kabisa kutekeleza Sheria ya Upataji wa Habari ya 2016.[19] Hakika mnamo tarehe 30 Septemba, Sheria hiyo ilitekelezwa.[20] Asasi za kiraia na mashirika ya serikali ya kimataifa yalipongeza serikali kwa kuchukua hatua hii mwafaka. Utekelezaji wa Sheria hii utaondoa utamaduni wa usiri, na utaifanya serikali kuwa wazi zaidi na kuwajibika kwa raia wake. Walakini, bado kuna changamoto nyinginezo ambazo zinahitaji kushughulikiwa kabla Sheria kuweza kufanya kazi kikamilifu. Kwa mfano, Ibara ya 7 cha Sheria hiyo hiyo inaagiza "kuanzishwa kwa Tume ya Habari ya Umma kusimamia utekelezaji wa Sheria hii".[21] Ila, hakuna chombo kama hicho kilichopewa jukumu la kufanya kazi hizo za uangalizi.




**"Majukwaa ya dijiti yakawa silaha dhidi ya wanawake"**

17. https://africaninternetrights.org/sites/default/files/Donald_Flywell-1.pdf
18. https://www.apc.org/en/pubs/tackling-gender-based-cyber-violence-against-women-and-girls-malawi-amidst-covid-19-pandemic
19. https://malawi24.com/2020/09/19/cso-hails-govt-for-operationalizing-ati/
20. https://www.nyasatimes.com/un-commends-malawi-for-operationalization-of-access-to-information-law/
21. https://www.right2info.org/laws/malawiaccesstoinfo.pdf/at_download/file

Cha msingi, kampuni za simu zinazoongoza nchini Malawi za TNM na Airtel ilipunguza bei za data za mtandao.[22] Airtel ilitangaza bei mpya ya upunguzaji wa hadi 40% na faida iliyoongezeka ya 588% mnamo 2019,[23] huku TNM pia ikipunguza bei za data mnamo Julai 30, 2020, licha ya kampuni hiyo kurekodi kupungua kwa faida ya 10% mnamo 2019 ikilinganishwa na 2018. Wakati wananchi wengine walizingatia kupunguzwa kwa bei ya data kama jambo la kusherekea, wengine walishutumu kuwa hatua hiyo hakuwa na manufaa yoyote ikizingatiwa kuwa athari yake hai kwa raia ilikuwa ndogo mno. Hata hivyo, kumekuwa na uboreshaji wa ushiriki wa raia mtandaoni kwa sababu ya kupungua kwa bei za data za mtandao.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Tukizingatia matukio haya, ni dhahiri shahiri kuwa 2020 ulikuwa wenye matukio mseto katika muktadha wa haki za kidijitali nchini Malawi. Ukiukaji wa haki za kidijitali kama vile gharama za juu za ufikiaji mtandao, unyanyasaji wa mtandaoni na dhidi ya wanawake na wasichana, ufuatiliaji wa vyombo vya dola mtandaoni, kutokuwepo kwa faragha ya kibinafsi mtandaoni na ulindaji data kunaendelea kutishia uhuru wa kujieleza wa raia katika nyuga za kidijitali. Huku kunaendelezwa zaidi na sera dhaifu na mifumo ya udhibiti, na matumizi ya sheria za kibabe zilizorithiwa kutoka enzi zote za ukoloni na wakati wa enzi za chama kimoja (1964-1994) ambazo bado hazijafutwa. Hata hivyo, uongozi wa serikali ya sasa chini ya Rais Chakwera, pia umetoa hakikisho kuwa vifaa vya mtandao na TEHAMA viwe nafuu na kuweza kufikiwa na Wamalawi wote. Hili limedhihirishwa kwa upunguzwaji bei za vifurushi vya mtandao, uendelezaji uanzishwaji wa vituo vya kutoa huduma za mtandao (telecenters) maeneo ya vijijini, utekelezaji wa Sheria ya Upataji wa Habari ya 2016, na mingineyo. Hivi karibuni, hakujakuwepo na visa vilivyoripotiwa vya uvumizi kwenye nyuga za raia ikilinganishwa na mwaka wa 2019. Kulingana na hitimisho hili, mapendekezo ni kama ifuatavyo:

- Serikali inapaswa kuunda kwa haraka sheria ya ulindaji data za kibinafsi ili kuhakikisha kuwa data za kibinafsi za umma zinalindwa katika maeneo nje na ndani mtandao.
- Serikali inapaswa kufuta sheria andamizi ambazo zinakiuka uhuru wa raia wa kujieleza mtandaoni kama vile Sheria ya Uchochezi, Kanuni za Adhabu, na Sheria ya Miamala ya Kielektroniki na Usalama wa Mtandaoni.
- Serikali inapaswa kupitia upya Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kupambana na aina zote za ukatili wa kijinsia na kujumuisha maswala ya ukatili wa kijinsia mtandaoni. Hii itahakikisha usalama wa wanawake na wasichana mtandaoni, na pale utovu wa nidhamu huo unapotokea utaratibu mzuri lazima uzingatiwe.
- Serikali inapaswa kuondoa tozo kubwa za ushuru zilizowekwa kwa uingizaji nchini wa vifaa vya TEHAMA ili kuhakikisha ufikiaji na unafuu wa huduma za TEHAMA kwa idadi ya watu waliotengwa. Hii itapunguza pengo la usawa wa kidijitali ambao upo sasa nchini.

22. https://cipesa.org/2020/08/malawi-telcos-reduce-data-prices-in-response-to-cipesa-chrr-campaign-2/
23. https://times.mw/airtel-profit-up-by-588/#:~:text=Malawi%20Stock%20Exchange%20recent%20entrant,by%20the%20company%20has%20shown.

# LONDA

**MALAWI HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI**

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

**Paradigm Initiative**
374 Borno Way, Yaba, Lagos, Nigeria
Email: media@paradigmhq.org
www.paradigmhq.org
@ParadigmHQ